# SHINYALU SOUTH CLUSTER

## KISWAHILI DARASA LA SITA (6) 2020

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

Msichana wa umri _1_ miaka _2_ alifariki jana kauntini marsabit _3_ ya kula mahindi ya msaada kutoka kwa wafadhili. Watu wengine _4_ wa familia yake _5_ ni pamoja na mamake walitibiwa kwa _6_ makali ya tumbo, katika hospitali kuu ya kaunti baada ya _7_ chakula _8_ kilichoshukiwa kuwa na sumu.

"Okech alifariki _9_ ndugu zake watatu walitibiwa kwa maumivu _10_ tumbo" alisema afisa mkuu wa polisi. Mvulana _11_ alifariki mwendo wa saa kumi za asubuhi baada yay eye na ndugu zake _12_ hospitalini kwa matibabu. Mkuu wa polisi alieleza kwamba wote walikuwa _13_ maumivu _14_ tumbo muda mfupi baada ya kula chakula cha jioni _15_ maumivu hayo yalizidi mchana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. wa | C. kwa | D. na |
| 2. | A. mitisa | B. tisini | C. tisa | D. stisa |
| 3. | A. badala | B. baadaye | C. labda | D. baada |
| 4. | A. watano | B. tano | C. mbili | D. mmoja |
| 5. | A. ambamo | B. ambao | C. ambalo | D. ambako |
| 6. | A. maumivu | B. uchungu | C. vindonda | D. mateso |
| 7. | A. kukula | B. kulia | C. kulila | D. kula |
| 8. | A. hiyo | B. hilo | C. hicho | D. huko |
| 9. | A. nayo | B. nao | C. baada | D. kabla |
| 10. | A. ya | B. la | C. kwa | D. mwa |
| 11. | A. huyu | B. hawa | C. huyo | D. hao |
| 12. | A. kufika | B. kufikiria | C. kufikisha | D. kufikishwa |
| 13. | A. wanalalamika | B. wamelalamika | C. wakalamika | D. watalalamika |
| 14. | A. za | B. la | C. ya | D. kwa |
| 15. | A. ingawa | B. ikawa | C. ilikuwa | D. itakuwa |

**Kutoka nambara 16-30 ,jibu kulingana na maagizo**

16. Andika tarakimu hii kwa maneno 8,659
    A. Mia nane mia sita na hamsini na nane
    B. Elfu nane mia tisa hamsini na tisa
    C. Elfu nane mia sita hamsini na sita
    D. Elfu nane mia sita hamsini na tisa



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

17. Nilipomwomba mwalimu wetu ruhusa ya kwenda msalani, alikataa kwa jino na ukucha ______

A. Katakata B.Ng'o

C.Hapana hapana D.Ng'a

18. Ni sentensi ipi iliyo sahihi

A. Shati lake ni nyeupe
B. Alipoesha chai kwa kikombe
C. Alituhadithia akiwa usingizini
D. Aling'orota akiwa usingizini

19. Hali ya kuwa mke au mume ni

A. JinsiB.Jinsia

C.Sinzia D.maumbile

20. Neno jicho liko katika ngeli ipi?

A. I-ZIB.JI-MA

C.A-WA D.LI-YA

21. Tegua kitendawili hiki

Nyumbani mwangu mna shetani ambaye daima anakunywa maji yangu

A. Shamba B.Mtoto

C.Taa D.mtungi

22. Ni nini maana ya semi hii; Chakula alichokipika kilikuwa asali.

A. Kilikuwa kitamu
B. Kilipikwa kwa viungo
C. Kilitiwa asali
D. Kiliwekwa nyuki

23. Tumia amba ipasavyo

Kipofu ______ tulimwona amerudi

A. AmbachoB.Ambaye

C.AmbakoD.aliye

24. Fupisha maneno haya wajomba zako

A. WajombakoB.wajombanu

C.Wajombazo D.mjombako

25. Nywele za mwilini zinazoota mgongoni, mikononi, miguuni na kifuani huitwa

A. Mvi B. nywele

C.Donya D. malaika

26. Kitenzi kunja katika hali ya kutendeana ni


A kunja kunja B. kunjia

C. kunjiana D. kunjisha

27. Ni sentensi ipi iliyo katika hali ya mazoea

A. mama hupika chakula kitamu
B. mama anapika chakula kitamu
C. mama atapika chakula kitamu
D. mama alipika chakula kitamu

28. Hili ni umbo lipi?



A. tao B. nusu duara

C. nusu kipenyo D. kipenyo

29. Ni vazi lipi kati ya haya livaliwalo na wanawake pekee

A. Kabuti B.kanchiri

C.Tai D.chupi

30. Chagua neno lifaalo

yeye ni yatima kwani hana baba ___ mama

A. ila B. kama

C. wala D. na

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.**

Ng'ombe ni mojawapo wa wanyama wanaofungwa na binadamu. Kuna ng'ombe wa kike na wa kiume. Binadamu huwalisha ng'ombe hawa kwa nyasi na vyakula vinginevyo ili wawe wenye afya nzuri. Wanyama hawa hupelekwa kwenye majosho ili wawe wenye afya nzuri.

Ng'ombe ndume hutumiwa kwa kazi za kinyumbani kama vile kulima, kukokota mikokoteni ma mapipa ya kuchotea maji. Kilimo ndicho uti wa mgongo wa taifa la kenya. Ng'ombe wanapomsaidia mwananchi katika kupanda na kupalilia mimea yake, bila shaka huwa wanainua uchumi wa taifa la kenya.Katika kilimo, mbolea ni muhimu. Wakulima wafugaji hutumia mbolea ipatikanayo kutoka kwa mifugo wao na kupunguza gharama ya ununuzi wa mbolea. Ng'ombe wa kike naye ana faida chungu



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Mob: 0734579299
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

nzima. Yeye hufugwa ili aweze kuzaa ndama huku kunazidisha idadi ya mifugo ya mfugaji. Ng'ombe azaapo humnyonyesha ndama wake ili awe mwenye afya. Maziwa haya pia hukamuliwa kama chakula cha binadamu na wanyama wengine kama paka. Mbali na kunywa maziwa pia huuzwa na kumpa mkulima mapato.Watu wengi pia hula nyama ya ng'ombe ambayo ina protini inayompa binadamu joto mwilini. Mbali na nyama, ng'ombe wanapochinjwa ngozi zao, mifupa na pembe pia huuzwa. Ng'ombe ni mnyama mwenye umuhimu katika maisha ya binadamu yoyote.

31. Kulingana na taarifa sababu maalum ya kuwalisha ng'ombe ni?
    A. Waweze kutoa maziwa
    B. Wawe wenye afya
    C. Waweze kutoa mbolea
    D. Waweze kuzaana
32. Ni kimelea yupi anayezuiliwa ng'ombe apelekwapo kwenye josho
    A. chawa B. mbu
    C. funza D. kupe
33. Ni faida ipi ya ng'ombe inayosaidia binadamu katika ukuzaji wa uchumi
    A. kilimo
    B. kutupa maziwa
    C. kwendo kwenye josho
    D. kuzaana
34. Ni madini yapi yanayopatikana ndani ya nyama ya ng'ombe?
    A. vitamini B. protini
    C. kashiamu D. chuma
35. Ni mnyama yupi wa nyumbani anayenufaika kutokana na ng'ombe
    A. Paka B.punda
    C.Mbuzi D.kondoo
36. Ni gharama ipi anayopunguziwa mkulima kulingana na aya ya tatu
    A. kununua maziwa
    B. kununua mbolea
    C. kununua ndama
    D. kununua nyama
37. Kati ya faida zifuatazo ni ipi ya ng'ombe ndume pekee?
    A. maziwa B. ngozi
    C.kilimo D. kuzoa
38. Kulingana na taarifa nchi ya Kenya hupata pato lake kuu kutokana na?
    A. Biashara B.lekezaji
    C.Uluguzi D. ukulima
39. Madhumuni ya kumnyonyesha ndama ni nini?
    A. Kuwa kwenye afya
    B. Kupata maziwa
    C. Kupata ngozi nzuri
    D. Afya kuzorota
40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni
    A. Wanyama wa nyumbani
    B. Ng'ombe wa kike
    C. Faida za ng'ombe
    D. Ng'ombe na ndama

**<u>Soma habari ifuatayo kasha ujibu maswali 40-50</u>**

Hapo kale paka hakukaa katika nyumba za watu. Alikaa mwituni au vichakani tu. Paka alikuwa rafiki wa sungura wa chanda na pete, paka alistaajabia werevu wa rafiki yake. Lakini siku moja mnyama aitwaye funo aligombana na sungura wakapigana hata fugo akamuua sungura kwa pembe zake.Paka akawa hana rafiki, akaonelea heri afuatane na huyo funo. Baada ya siku chache wakapambane na chui ambaye alimshika fune akamuua na kumla paka akaingiwa na huzuni akakata shauri kufanya urafiki na chui. Kwa bahati mbaya urafiki huo haukudumu kwa muda mrefu kwa sababu ugomvi ulizuka baina ya chui na samba wakapigana. Katika



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

mapigano hayo akauawa na samba.Paka akafikiri ya kwamba rafiki ambaye angalimfaa sana ni samba. Siku moja tembo alifika pale walipoishi, akachokoza simba kwa maneno makali. Samba akakasirika sana, hapo vita vikali vikaanza. Samba akashindwa na tembo. Paka akasema kuwa rafiki bora ni Yule mshindi mapambanoni. Papo hapo akamwacha samba na kufuatana na tembo.

Kabla hawajafika mbali wakakutana na mwindaji aliye kuwa tayari na silaha zake. Bila kuchelewa Yule mwindaji aliyemlenga tembo kwa mshale wa sumu. Maskini tembo akafariki. Paka akamuona mwindaji kuwa rafiki wa dhati.Wakashika safari ya kwenda nyumbani. Mwindaji alipofika nyumbani akalakiwa na mkwe huindo lake na silaha. Paka akaona vile na kuzidi kushangaa. Akadhani kwamba mwanamke ndiye aliyekuwa na nguvu kuliko wote kwa sababu aliweza kumpokonya mwanamme aliyemuua tembo silaha na windo lake. Basi paka akamfanya mwanamke rafikiye na kumfuata kwenda jikoni. Tangu siku hiyo paka huishi nyumbani.

41. Aliyekuwa rafiki mwerevu wa paka ni ____
    A. Simba B.Tembo
    C.Sungura D.mwanamke
42. Funo alitumia nini kumuua sungura?
    A. Kwa kumkatakata
    B. Kwa kutumia pembe zake
    C. Kwa kumnyonga
    D. Kwa kutumia makucha yake
43. Mfuko wa mshale huitwaje?
    A. Podo B.Chembe
    C.Kigumba D.uta
44. Paka alifanya urafiki na wanyama wangapi
    A. watatu B. wanne
    C. wawili D. watano
45. Paka alifikiria nini alipoona mke wa mwindaji akichukua silaha za mumewe?
    A. Kuwa mwanamke ndiye aliyekuwa na nguvu kuliko wanyama wote
    B. Kuwa mwanamume amenyang'anywa na mwanamke
    C. Kuwa mwanamke alikuwa akitaka kumuua mumewe
    D. Mwanamke alinuia kumchoma na kumkatakata
46. Ni mnyama gani aliyemuua chui
    A. TemboB.Funo
    C.BinadamuD.simba
47. Unafikiri ni kwa nini paka alizoea kuacha marafiki zake
    A. alizoea kucheza na marafiki wapya
    B. alipendelea rafiki aliyekuwa mshindi katika mapambano
    C. alipendelea kuishi pekee
    D. alifukuzwa na rafiki zake kwa kukosa ujasiri
48. Mwindaji alituma _____ kumuua tembo
    A.mkuki B.panga
    C. mshale wa sumu D.bunduki
49. Methali inayoweza kutumika kueleza kisa hiki ni
    A. tama mbale mauti nyuma
    B. mla mawe hafi nawe ila mzaliwa nawe
    C. akili nywele kila mtu ana zake
    D. mwenye nguvu mpishe
50. Kichwa mwafaka cha habari hii ni?
    A. Paka na mwindaji
    B. Sababu yap aka kuishi nyumbani
    C. Paka na mwanamke
    D. Paka mwerevu



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com